

## GRADE 4 MID TERM 2 2020

### KISWAHILI

#### SEHEMU A:

1. **Soma jozi zifuatazo za maneno mwalimu akikusikiliza. (alama 3)**  
(a) ~~kamba~~, gamba. (b) chambo, jambo. (c) banda, panda.

2. **Soma vitanzandimi vifuatavyo mwalimu akikusikiliza. (alama 4)**  
(a) Baba alimvuta papa kwa kamba iliyokuwa karibu na gamba.  
(b) Jana nilizichana nywele kisha nikatoa doa kwenye nguo.

3. Andika majibu ya maamkuzi haya. (alama 3)

- (a) Shikamoo \_\_\_\_\_  
(b) Hamjambo \_\_\_\_\_  
(c) Salaam aleikum - \_\_\_\_\_

4. Tugua vitendawili. (alama 3)

- (a) Nifungue nikufunike \_\_\_\_\_  
(b) Ukinitembelea nyayo zi salama \_\_\_\_\_  
(c) Popote niendapo ananifuata \_\_\_\_\_

5. Tunga sentensi ukitumia maneno haya. (alama 2)

- (a) Kujifungua \_\_\_\_\_  
(b) Kwenda msalani \_\_\_\_\_

#### SARUFI.

1. Tunga sentensi ukitumia maneno haya. (alama 2)

- (a) Kochi \_\_\_\_\_  
(b) Neti \_\_\_\_\_

2. Tambua kwa kupigia mistari vitenzi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

- (a) Mtoto anakula chakula.  
(b) Wanafunzi wale wanasoma.

3. Tambua kwa kupigia mistari vivumishi katika orodha hii. (alama 2)  
Mtoto, kizuri, ruka, tembea, yule, safi, kijiko, mmoja, nyumba, darasa.

4. Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo. (alama 2)

- (a) wengi \_\_\_\_\_  
(b) hivyo \_\_\_\_\_

5. Tambua aina za maneno yaliyopigiwa mistari. (alama 2)

- (a) Mama anatembea polepole. \_\_\_\_\_  
(b) Tutaenda shuleni asubuhi. \_\_\_\_\_

6. Jaza nafasi kwa viunganishi sahihi. (alama 2)  
(lakini, na, kwa sababu)

- (a) Mtoto analia \_\_\_\_\_ ameanguka.  
(b) Nilienda kwao \_\_\_\_\_ sikumpata.

7. Tumia vihisishi vifuatavyo kutunga sentensi. (alama 2)

- (a) Lo!  
(b) Oyee!

8. Tumia vihusishi vifuatavyo kujaza nafasi. (alama 2)

- (a) Babu ameketi \_\_\_\_\_ mti. (ndani ya, chini ya)  
(b) Maji yamejaa \_\_\_\_\_ glasi. (ndani ya, juu ya)

9. Andika wingi wa maneno haya. (alama 2)

- (a) Chura \_\_\_\_\_  
(b) Daktari \_\_\_\_\_

10. Andika umoja wa sentensi hii. (alama 2)  
Watoto wameenda kuwaona maseremala.

11. Chora vifaa vifuatavyo na uvipake rangi.

(a) Kinu na mchi (alama 3)	(b) Rinda (alama 3)

**SEHEMU B:**

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuata.**

Mzee Ojwang' ni mzee mwenye bidii sana. Yeye hufanya kazi ya useremala. Katika karakana yake, yeye hutengeneza meza, makochi, na vifaa vingine. Yeye hupenda kuvaa bwelasuti ili nguo zake zisiwe chafu. Pia huvaa chepeo kuzuia ukali wa miale ya jua. Ameijenga nyumba yake upande wa kusini wa shule ya Jahari. Nyumba hiyo ina vyumba kama vile sebule, msala, jikoni na vyumba vya kulala.

Kila jioni Mzee Ojwang' na familia yake ya watu watatu, watoto wawili na mke mmoja hukutana ili kula. Chakula hicho huwa kitamu kama asali. Kila mmoja hunawa kwa maji safi na sabuni kabla ya kula. Watoto husubiri wazazi wanawe kwanza ndipo nao wanawe. Kila mtu hula akiwa amenyamaza. Wanaelewa kuwa kuongea na chakula mdomoni ni tabia mbaya. Baada ya kula, wote hunawa. Watoto huondoa vyombo mezani kisha wakamsaidia mama yao kuviosha. Baadaye wao huenda vitandani na kulala fofofo.

**Maswali**

(a) Andika vifaa viwili ambavyo Mzee Ojwang' hutengeneza katika karakana yake (alama 2)

- (i) \_\_\_\_\_  
(ii) \_\_\_\_\_

(b) Kwa nini Mzee Ojwang huvaa mavazi yafuatayo (alama 2)

- (i) Bwelasuti \_\_\_\_\_  
(ii) Chepeo \_\_\_\_\_

(c) Nyumba ya Mzee Ojwang hupatikana upande upi wa shule ya Johari? (alama 2)

(d) Mzee Ojwang ana watoto wangapi? (alama 1)

(e) Andika mambo mawili ambayo hufanywa kabla au wakati wa kula yanayoonyesha nidhamu (alama 2)

- (i) \_\_\_\_\_  
(ii) \_\_\_\_\_

(f) Andika mambo mawili ambayo hufanywa baada ya kula na familia ya Mzee Ojwang. (alama 2)

- (i) \_\_\_\_\_  
(ii) \_\_\_\_\_

